

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baiskeli Dar es Salaam**  
**Tarehe 25 februari 2006**

**Waliohudhuria**

Elaine Baker

Frank Mwasa

John Emil Maximilian

Juma Ali Salehe Jongo

Salum Chimburumburu

Selemani Alonasi

**Usajili**

Elaine Baker alitoa maendeleo ya mwenendo wa Usajili. Ofisi ya makamu wa Rais (Usajili wa NGO kwa sasa unafanywa na Wizara ya Jamii, Jinsia na Watoto) imekubali ombi letu lakini bado tunahitaji barua kutoka mkoa wa Dar es Salaam. Ofisi ya makamu wa Rais itatupa barua ya utambulisho ili ipelekwe Ofisi ya mkoa. Ilikubalika kuwa Juma Jongo atachukua barua hiyo jumatatu, Elaine ataandaa nyaraka nyingine na watakutana kwenye ofisi za mkoa Ilala Boma.

**Kazi**

Matangazo yalisomwa lia ilikubalika kungoja usajili kabla ya kuyatoa.

Nakala za vipeperushi visemavyo "kila jumamosi" badala ya tarehe viligawanywa na Elaine. Ilikubalika kwamba wajumbe watatoa nakala na kuzigawa.